# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MOROGORO

**MEI, 2025**

**MOROGORO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za Simu:
**Mkuu wa Shule** 0762 559 133
**Makamu Mkuu wa Shule** 0713 661 815/0768 951 333
**Matron** 0716 901 116
**Barua pepe:** **morogorosecondary2018@gmail.com**

Shule ya sekondari Morogoro,
**S.L.P 240,**
Morogoro.

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MOROGORO ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO MKOANI MOROGORO MWAKA 2025**

**UTANGULIZI**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii **mwaka 2025** na atasoma tahasusi ya …………. Shule ya Sekondari Morogoro ni Shule ya kutwa kwa wavulana na bweni kwa wasichana.

**MAHALI SHULE ILIPO**

**Shule ya Sekondari Morogoro** ipo umbali wa **Kilometa 4** kutoka kituo kikuu cha mabasi Msamvu Mashariki mwa Mji wa Morogoro ambapo Usafiri wa mabasi madogo kutoka Msamvu unapatikana nje ya kituo cha mabasi. Hivyo nauli ni **Shilingi 3,000/-** kwa pikipiki na **Shilingi 5000/-** kwa bajaji.

**MIHULA YA MASOMO**

Muhula wa Masomo unaanza **tarehe 08/07/2025** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **07/08/2025** kuanzia saa nne asubuhi hadi

saa kumi na mbili jioni ambapo wavulana wataripoti **tarehe 08.07.2025** saa moja kamili asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.07.2025**

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

**Zingatia maelekezo yote yanayohusiana na sare za Shule ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza. (Namba ya Mwalimu wa uniform ni 0713471465)**

**Wavulana**

- Mashati mawili (yanapatikana shuleni)
- Suruali mbili na tai (vinapatikana shuleni)
- Raba za Michezo rangi nyeusi
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na kisigino kirefu na urembo wowote
- Soksi pair tano (zinapatikana shuleni)
- Fulana mbili zenye nembo ya Shule (zinapatikana shuleni).
- Mkanda wa Suruali mweusi wa ngozi usio na urembo wala mpana zaidi ya sentimita tatu.
- Sweta la Shule (linapatikana shuleni)

**Wasichana**

- Sketi mbili (zinapatikana Shuleni).
- Mashati mawili yenye nembo na tai (vinapatikana Shuleni)
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi visivyo na Urembo wowote
- Soksi nyeupe pair tano (zinapatikana Shuleni)
- Fulana mbili zenye nembo ya Shule (zinapatikana Shuleni)
- Sweta la Shule (linapatikana shuleni)
- Hijabu na nusu kanzu (vinapatikana Shuleni)
- Truck suit (inapatikana shule)
- Nguo za kushindia (shamba dress) mbili (zinapatikana Shuleni)
- Shuka nne na foronya zake (zinapatikana Shuleni)

### 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 11 (counter Book) quire 3 au 4, kalamu za risasi, wino na mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set). (Kwa wanafunzi wa EGM, HGE na ECA)

ii. Madaftari 11 (counter Book) quire 3 au 4, kalamu za risasi na za wino (Kwa wanafunzi wa (HGL, HKL, KEC, HGK)

iii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa kila muhula aina no 1, Golden Star, dolphin premium au A4

iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ***(Ipo mwisho)***

v. Scientific Calculator (**non programmable** calculator) iwe (fx-991). Hii ni kwa wanafunzi wanaosoma ECA, HGE na EGM.
vi. Godoro lenye upana wa futi 2 1/2
vii. Blanketi moja
viii. Mto mmoja wa kulalia
ix. Nguo za ndani za kutosha
x. Night dress mbili
xi. Kanga/kitenge doti moja na taulo kwa ajili ya kuogea
xii. Chandarua cha rangi nyeupe pembe nne
xiii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xiv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xv. Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dini yako

*Angalizo:Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani zaidi ya zilizotajwa hapo juu.*

## VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA VYA KUJA NAVYO

**Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi shuleni;**

- **Soft bloom moja**
- **Squizer moja**
- **Hard bloom moja**
- **Mfagio wa chelewa mmoja**
- **Sabuni ya maji aina ya (Arrow) 3 litres**

**Wanafunzi wa michepuo/tahasusi zifuatazo HGL na ECA waje na kwanja /fyekeo moja**

**Wanafunzi wa michepuo/tahasusi za HKL na KEC waje na Jembe moja lenye mpini imara.**

**Wanafunzi wa michepuo/tahasusi za EGM na HGK waje na Panga moja**

**Wanafunzi wa mchepuo/tahasusi ya HGE waje na Ndoo kubwa mbili za litre 20 (ziwe za mafuta)**

### 1.3 Michango mbalimbali

**a) Wanafunzi wa Bweni (Wasichana)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Ulinzi | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Wanafunzi wa Kutwa (Wavulana)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Ulinzi | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**NB**:- *Pamoja na taarifa hii napenda kukujulisha kuwa malipo yote yalipwe benki kama ilivyoainishwa kwenye jedwali bila kupungua,* ***Original Bank Pay Slip*** *iletwe kwa Mhasibu ikiwa na jina la mwanafunzi, kidato chake na ikionesha* ***Tahasusi (combination)*** *aliyochaguliwa. Jina la akaunti Morogoro Secondary School, akaunti namba* ***22101100145*** *NMB.* ***HATUPOKEI FEDHA TASLIMU.***

Aje na Tsh 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka mzima (kwa wale ambao hawana bima ya afya). **BIMA YA AFYA NI LAZIMA** kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka mzima sehemu yoyote nchini. (fedha hizo siyo sehemu ya michango ya shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule)

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba wa wazazi au Ugonjwa sugu tu**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 3 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vinasaba vyake kama chaja, line au betri redio na flash katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kutofanya mitihani ya ndani na nje ya shule.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Aje na kivuli cha **matokeo (photocopy) result slip** na **cheti cha kuzaliwa** vikiwa kwenye **flat file (faili)** aina ya ngalawa la karatasi ngumu (**Lisiwe la plastic**). Pia fomu zote zilizojazwa zibanwe kwenye faili hili na kukabidhiwa kwa msajili wa wanafunzi.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KIAMBATANISHO 'A'**

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
## SHULE YA SEKONDARI MOROGORO

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**Picha mwanafunzi**

(a) **Ijazwe na mwanafunzi**:

1. Jina kamili la mwanafunzi ____________________
2. Uraia ____________________
3. Dini ____________________
4. Tarehe ya kuzaliwa ____________________
5. Mkoa aliozaliwa ____________________
6. Wilaya aliyozaliwa ____________________
7. Yatima/Siyo yatima____________________
8. Kata unayoishi____________________

8. Shule alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya morogoro

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/ SEKONDARI | TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA | TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA |
|---|---|---|---|
| 1. | 1. | 1. | 1. |
| 2. | 2. | 2. | 2. |
| 3. | 3. | 3. | 3. |
| 4. | 4. | 4. | 4. |

(b) **Maelezo binafsi ya mzazi / mlezi**

**Picha mzazi/mlezi**

Jina kamili la Mzazi / Mlezi ____________________

1. Uraia ____________________
2. Anuani kamili ____________________
3. Sehemu unayoishi ____________________
4. Mtaa ____________________
5. Namba ya nyumba ____________________
6. Namba ya simu ____________________(ya haraka)
7. Kazi ya mzazi ____________________(Mfano
8. Jina la Mwajiri na Idara ____________________

- Anuani : ______________________________________________
- Namba ya simu : _______________________________________

**FOMU YA MZAZI YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE**

**KIAMBATANISHO 'B'**

Mkuu wa Shule,
Sule ya Sekondari Morogoro,
S.L.P. 240,
**MOROGORO.**

Picha ya Mzazi / Mlezi

| |
|---|
| |

**YAH: AHADI YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE**

Mimi __________________________________________________ Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi_______________________________________________ wa kidato cha **Tano** katika Shule ya Sekondari ya Sekondari Morogoro, nathibitisha kuwa nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote ya shule. Naahidi pia kumsimamia mwanangu afuate sheria, kanuni na taratibu za shule. Naahidi pia kutoa ushirikiano na shule kwa manufaa ya mwanangu na kulipa michango kwa wakati.

**NB:- LIKIZO UNGETAMANI MWANAO AENDE WILAYA**

**YA..............MKOA....................JINA LA**

**ATAKAYEMPOKEA.....................................UHUSIANO.............................................SIMU**

**..................................**

**PICHA ZA NDUGU WA KARIBU WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANANGU:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

**SIMU.......................Simu..........................Simu.............................Simu..........................**

**Jina la Mzazi / Mlezi :** ____________________________________________

**Sahihi ya Mzazi / Mlezi :** ________________________________________

**Namba ya simu:** ________________________________________

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KWENYE MIGOMO NA KUTOKUWA NA MAKOSA YA JINAI**

**KIAMBATANISHO 'C'**

Mkuu wa Shule,
Sule ya Sekondari Morogoro,
S.L.P. 240,
**MOROGORO.**

PICHA

**YAH: AHADI YA MWANAFUNZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE**

Mimi________________________________________ Mwanafunzi wa kidato cha **Tano tahasusi ya......................** katika Shule ya Sekondari ya Sekondari Morogoro, nathibitisha kuwa nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote ya shule. Naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule. Naahidi pia kutoa ushirikiano kwa shule kwa manufaa ya shule na nitakuwa kinyume na matendo yote yanayovunja na kuhatarisha amani ya shule (fujo na migomo). Nitakuwa tayari kuwajibika kwa mujibu wa sheria za shule endapo nitakwenda kinyume na sheria za shule.

Endapo nitaharibu miundombinu ya shule kwa namna yoyote ile nitakuwa tayari kuwajibika ikiwa ni pamoja na kufidia hasara yoyote ile itakayokuwa imejitokeza kwa kusababishwa na mimi.

**Jina la Mwanafunzi:** ________________________________________

**Sahihi ya Mwanafunzi:** ________________________________________

**Namba ya simu ya mzazi:** ________________________________________

**KIAMBATANISHO 'D'**

*Morogoro Secondary School*
*P. O. Box 240, Morogoro .Mobile 0689639053*

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the candidate)**

Surname………………………… Other names……………………….. ……………………………..

Age ……………… Sex…………… Combination……………… School……………………………

**PART II: PERSONAL HISTORY (To be filled by medically qualified and registered professional)**

Are you suffering of have you suffered from any of the following? Indicate **Yes** or **No**

1. Tuberculosis…………………………… Epilepsy………………………….
2. Asthma……………………............... Deformity……………………….
3. Rheumatic fever……………………… Mental illness………………….
4. Allergic disorders…………………… Eye disorder…………………….
5. Heart disease………………………….. Ear, Nose, Throat disorder……………
6. Gastric or duodenal ulcers………….. Skin disease……………………..
7. Jaundice ……………………………… Anemia………………………….
8. Dysentery…………………………… Varicose veins…………………
9. Kidney disease…………………….. Diabetes…………………………
10. Gynecological disorder………………. Any other serious disorder (specify)…………….

**PART III: PHISICAL EXAMINATION**

1. Height (cm) ……………………………...
2. Skin…………………………………………..
3. Weight (kg)……………………………….
4. Eyes: Conjunctive…………………….. Pupil……………… Vision

Right……………………………………. Left………………..

5. Ears (state if any discharge)………………. Mouth/throat………………
6. Nose…………………………… Respiratory system……………………………
7. Abdomen…………………….. Any abnormality………………………………..
8. Cardiovascular system………………. Blood pressure ………………………………..

Systolic ……………………………………… Diastolic…………………………………

Heart: Any murmur ………………………………… Arteries veins ……………………

**PART IV: LABORATORY**

1. Urine: Albumin…………………………… Sugar………………….

Leucocytes………………… Schistosoma…………………. …………………………

2. Stool: Special emphasis on hookworms or schistosoma………………………………..

3. Blood examination

a) Hb level……………………………………
b) Neutrophil…………………………………
c) Eosinophils……………………………....
d) Basophiles…………………………………..
e) Lymphocytes………………………………..
f) Monocytes…………………………………..
g) ESR…………………………………………

4. X – Ray examination: Chest (include Radiologist's report)………………………….
5. Serology Widal test …………………… VDRL……………………………………
6. Pregnancy test…………………………

**PART V: CONCLUSION**

I have examined (**name**)…………………………………. and consider that he/she is physically and mentally fit/not fit to be admitted for secondary education.

Name…………………………………….. Title……………………..
Qualification…………………………….. Signature………………….
Date……………….. Address………………………..
....................................................
....................................................

## UTANGULIZI

Simu ni nini? Simu ni chombo cha mawasiliano kinachotumia/kupokea mawimbi ya sauti kwa njia ya kieletroniki. Simu inayokusudiwa katika maelezo haya ni simu ya mkononi ambayo inajumuisha vipuri vya simu kama vile betri, “headphone”, laini na kasha la simu.

## UMUHIMU WA MAWASILIANO YA SIMU

Kwa kuwa simu inaendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivyo matumizi yake kwa kiwango fulani hayaepukiki kwa takribani watu wa rika zote. Hata hivyo, matumizi ya simu kwa rika la wanafunzi yana madhara makubwa hivyo sharti yadhibitiwe ili kuleta matumizi yenye tija. Shule kwa kutambua umuhimu wa simu imeweka utaratibu rasmi wa matumizi ya simu kwa wanafunzi. Mkuu wa shule ameiteua rasmi ofisi ya malezi kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi kupata mawasiliano na wazazi pale inapohitajika na chini ya uangalizi maalumu. Uzoefu unaonesha kuwa wanafunzi wasiposimamiwa kikamilifu na walimu ambao wana fahamu tabia zao kwa undani wanaweza kutumia simu hizo za walezi kufanya udanganyifu na kuathiri maendeleo yao kitaaluma. Maelezo haya yunanatoa angalizo kuwa ni muhimu sana matumizi ya simu yasimamiwe kikamilifu.

## ATHARI ZA MATUMIZI YA SIMU KWA WANAFUNZI

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa shuleni hapa kwa muda mrefu sasa, utafiti ulijaribu kuhusianisha athari za simu kwa maendeleo ya taaluma kwa wanafunzi wa kidato cha I hadi VI utafiti uling’amua athari zifuatazo:-

i. Kwa kuwa simu haziruhusiwi shuleni kwa mujibu wa kanuni na sheria za uendeshaji wa shule mwanafunzi mwenye kumiliki simu anakuwa kwenye hali ya wasiwasi wakati wote akihofu kukamatwa na simu hivyo anakosa utulivu ambao ni muhimu sana kwa mazingira ya kujifunza.
ii. Mwanafunzi mwenye simu anatumia nguvu na akili nyingi sana kutafuta sehemu ya kuficha simu, maarifa hayo yangetumika darasani yangeweza kuleta tija kubwa sana katika taaluma.
iii. Utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 95% ya wanafunzi wenye kumiliki simu wanazitumia simu hizo kwa ajili ya kujenga na kudumisha mahusiano ya kimapenzi na wenzao au watu wenye umri mkubwa kuliko wenyewe. Hali hii huathiri taaluma na ufaulu wa mwanafunzi kwa ujumla.
iv. Taarifa/ujumbe wa kimapenzi huwaathiri wengi kwa kuwa wanatumia muda mrefu kutafakari na kutafuta majibu yenye mshindo mkubwa ya kumrudishia mtumiaji wa awali. Vile vile ujumbe wa kimapenzi huathiri wanafunzi wengi kwa kudhani kuwa jumbe hizo ni za kweli ili hali nyingi ni za uongo na za kuwaghilibu.
v. Wanafunzi wenye kumiliki simu za mikononi hutumia muda mwingi wa usiku “kuchat” (kutumia jumbe fupi) badala ya kulala ili wapate nguvu ya kuamka asubuhi au usiku kujisomea. Hivyo wanafuzi wengi wenye simu huwa wachovu siku inayofuata, wanashindwa kumaliza kazi za nyumbani (home work) hivyo simu inachangia kurudisha nyuma maendeleo yao ya kitaaluma.
vi. Simu hurahisisha mawasiliano baina ya wanafunzi na wale wenye nia ya kuwalaghai wanafunzi wa kike kimapenzi kwa kuwa huweza kufanya ushawishi wao wakati wa usiku. Ikumbukwe kuwa wakati wa usiku mwili ukiwa umetulia hisia hutawala. Simu inaweza kumfanya mwanafunzi afikiwe na watu wasio na nia nzuri wakati wowote ule.
vii. Utafiti wetu umeng’amua kuwa simu zinasababisha wanafunzi wengi kutoroka vipindi wakati wa mchana na usiku ili wapate fursa ya kuweza kufanya mawasiliano na wenzao mbali na wanafunzi wema ambao huweza kutoa taarifa kwa walimu. Utoro wa aina hii umegunduliwa kwa wanafunzi wa kutwa wenye kutoroka vipindi wakati wa mchana na kujificha chooni ili waweze kuzungumza na rafiki zao wa kiume. Vile vile kwa upande wa bweni hufanya hivyo hivyo wakati wa mchana na usiku.

viii. Wanafunzi wengine wenye simu huzitumia simu hizo kuweka nyimbo za kusikiliza kwa muda mrefu.

ix. Kwa kuwa wanafunzi hununua simu hizo wenyewe au hununuliwa na watu wasiokuwa wazazi wao hivyo gharama za uendeshaji simu hizo hupelekea baadhi yao kurubuniwa kirahisi au kuwa wadanganyifu kwa wazazi wao.

x. Wanafunzi wengi hutumia simu kuangalia picha za ngono, mpira na kufanya mawasiliano kwa njia za ‘twitter’, ‘face book’ you tube’ n.k. mawasiliano ya aina hii huathiri sana akili zao pamoja na maendeleo yao ya kitaaluma.

**KIAMBATISHO E**

**ADHABU KWA WANAFUNZI WENYE KUMILIKI SIMU**

Hivyo kwa kuzingatia madhara hayo Bodi ya Shule katika kikao chake cha tarehe 09.03.2013 iliamua kutolewa adhabu kali ikiwa ni:

**Kufukuzwa shule** kwa mwanafunzi atakayekutwa na kosa la kumiliki simu **au kifaa chochote cha simu kama betri, "headphone", line au kasha lake.**

Ninaleta kwako maelezo na kiapo hiki ili lolote litakalotokea kusiwepo na lawama.

**A. MWANAFUNZI**

***KIAPO CHA KUKUBALI MAELEKEZO KUHUSU SIMU***

Mimi ________________________________________ kidato cha ________________
Ninakubali maelekezo ya shule ya Sekondari Morogoro nikiwa mwanafunzi wa bweni/kutwa. Ninakubali masharti yote na ninaahidi kufuata utaratibu huo. Nipo tayari Uongozi wa Shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa shule kama nitatenda kinyume na maelekezo haya.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI __________________________ TAREHE ________**

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi _________________________ Mzazi/Mlezi wa ______________ wa kidato cha _____________________ nimesoma/nimesomewa na kuyaelewa maelezo yote kuhusiana na matumizi ya simu kwa mtoto wangu na nipo tayari kwa mwanangu kufukuzwa shule iwapo atapatikana na umiliki/kutumia simu bila ya uangalizi maalumu.

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI_________________________ TAREHE ____________**

## Tanbihi

- ❖ Kwa wanafunzi wa bweni tu; Mwanao anatakiwa kuja na sanduku la chuma dogo moja tu (tranka). Hatutampokea mwanafunzi mwenye mizigo mingine zaidi ya sanduku la chuma. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa. Endapo mwanafunzi atakutwa na nguo za nyumbani, nguo hizo zitanyang'anywa.
- ❖ Pia mwanafunzi hataruhusiwa kuja na chakula cha aina yoyote. Soda, juice, pipi, ubuyu pamoja na biskuti haviruhusiwi kabisa.

# VITABU VINAVYOTAKIWA KUNUNULIWA

## 1. GENERAL STUDIES

**1.1.** Understanding General Studies - by Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratias.

## 2. ECONOMICS

**2.1.** Jhinghan M. L. Principles of Economics: Macro & Micro Economic Theory. Current Edition.

2.2. Microeconomics for Advanced Secondary School – Student's book. Form Five.

2.3. Macroeconomics for Advanced Secondary School – Student's book. Form six.

By Tanzania Institute of Education (2022).

2.4. Principles of Economics. By Dwired D. N. (2022)

2.5. Modern Economics. By Robert Mduda.

2.6. Essentials of Economics for Advanced A Level: Paper 1 & 2. By Ambrose Adhiambo.

## 3. COMMERCE

**3.1.** Essentials of Commerce in East Africa by S. A. Butt

3.2. Commerce its Theory and Practice by Evelyn Thomas

3.3. A text book of Commerce by J. C. Singha and V.N. Mugali

3.4. A text book of commerce by Dinah Kamasanyu

## 4. ACCOUNTANCY

**4.1.** Advanced Financial Accountanting - Simplified Vol. 1. By N. A. **Saleemi.**

**4.2.** Advanced Financial Accountanting - Simplified Vol. 2. By N. A. Saleemi.

4.3. Business Accountong. Vol 1. By Frankwood

4.4. Business Accountong. Vol 2. By Frankwood

4.5. Review Questions. By Maheshwari Paper 1&2

4.6. Tanzania Institute of Education - Advanced Level Accountancy

## 5. GEOGRAPHY

**5.1.** Collin Buckle - Landforms in Africa

5.2. John M. Pritchard - Practical Geography for Africa

5.3. D. T. Msabila - An Intergreted Regional Study on Human and Economic **Geography. Advanced Level Paper 2.**

**5.4.** D. T. Msabila - A Comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary Schools.

5.5. R. B. Burnet - Physical Geography in Diagrams.

**6. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

**6.1.** Tanzania Institute of Education (2019) Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools.

**7. ADVANCED MATHEMATICS**

**7.1.** Non Programmable Scientific Calculator

7.2. Tanzania Institute of Education

**8. HISTORY**

**8.1** Idrissa Ramadhan Msuya - Learning Advanced African History

8.2 Tumaini C. K. & Shibitali (2017) Contemporary Historical Events. Advanced Level History One.

**8.3** Walter Rodney. How Europe Under developed Africa.

8.4 Magoti, B. Fundamental Principles of History One, A Captivating Guide to A Level Students. Paper 1 & Paper 2.

**8.5** Nomal Lowe (2013). Mastering Of Modern World History.

8.6 Jovitus Mwijage ( ). Major Events in African History.

8.7 Yassin Saleh (2018). Essentials in Advanced Level History Paper 1 & Paper

**9. KISWAHILI**

**9.1. Kiswahili 1.**

**9.1.1.** Kitangulizi cha tafsiri: Nadharia na Mbinu - By Kirangi

9.1.2. Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo - By F. Nkwera.

9.1.3. Historian a Matumizi ya Kiswahili - By M. Msokile

9.1.4. Kilangi Enock Lucas - Kiswahili 1 Shule za Sekondari.

**9.2. Kiswahili 2**

**9.2.1.** Nadharia ya Fasihi

9.2.1.1. Kilangi Enock Lucas - Kiswahili 1 Shule za Sekondari.

9.2.1.2. Fasihi ya Kiswahili - By M. M. Mlokozi

**1.1.1. Ushairi**

**1.1.1.1.** Kimbunga - By H. Gora

1.1.1.2. Mapenzi Bora - By S. Robert

1.1.1.3. Chungu Tamu - by T. A. Mvungi

1.1.1.4. Fungate ya Uhuru - M. S. Khatibu

**1.1.2. Riwaya**

**1.1.2.1.** Vuta N'kuvute - By S. A. Shafi

1.1.2.2. Mfadhili - By Hussein Tuwa

1.1.2.3. Kufikirika - By S. Robert

1.1.2.4. Usiku Utakapokwisha - By M. Msokile

**1.2. Tamthiliya**

**1.2.1.** Morani - By E. Mbogo

1.2.2. Kivuli kinaishi - By S. Mohamed
1.2.3. Kwenye Ukingo wa Thim - By E. Hussein
1.2.4. Nguzo Mama - By P. Muhando

## 2. ENGLISH LANGUAGE

### 2.1. LANGUAGE 1

**2.1.1.** Advanced Level English Language 1 For 5 & 6. By James E. Kinunda & Shadrack Ndambo
**2.1.2.** Advanced Level English Language 1 For 5 & 6. By Nicholaus Asheri

### 2.2. LITERARY THEORY

**2.2.1.** Advanced Level English Language II - By Gwama D. L.

### 2.3. PLAYS

**2.3.1.** Betrayal in the City - Francis Imbuga
2.3.2. I Will Marry When I Want - Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii
2.3.3. An Enemy of the People - Henrik Ibsen
2.3.4. Black Mamba - John Ruganda

### 2.4. SHORT STORIES

**2.4.1.** Encounters from Africa - Macmillan Education Limited

### 2.5. NOVELS

**2.5.1.** The Beautyful Ones Are Not Yet Born - Ayi Kwei Armah
2.5.2. A Man of the People - Chinua Achebe
2.5.3. The Rape of the Pearl - Magala Nyago
2.5.4. Vanishing Shadows - Namige Kayondo
2.5.5. His Excellency the Head of State - Danny Safo
2.5.6. A Season of Waiting - David Omowale

### 2.6. POETRY

**2.6.1.** Selected Poems - Tanzania Institute of Education
2.6.2. The Wonderful Surgeon and other Poems - Charles Mloka

**Tanbihi**

**Masomo mawili (2) ya lazima kwa wanafunzi wa kidato cha tano ni Historia ya Tanzania na Maadili na Academic Communication. Vitabu vilivyopo kwa ajili ya hayo masomo mawili ni vile vilivyoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule** 0762 559 133
- **Makamu Mkuu wa Shule** 0713 661 815/ 0768 951 333
- **Mwandamizi Taaluma** 0719 742 555/0652 681 848
- **Mwandamizi Malezi** 0654 451 331

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**BONEPHACE WEREMA GONJO**

